JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mkuu wa TAKUKURU (M),
Mtaa wa Viwandani,
S.L.P 306,
39101BARIADI, SIMIYU.
Simu: (028) 2700374 Nukushi (028) 2700532
Barua pepe: *rbcsimiyu@pccb.go.tz*
Wavuti: www.pccb.go.tz

APRILI, 2022.

TAKUKURU SIMIYU YAFUATILIA MIRADI YA MAENDELEO YA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI TATU

1. UTANGULIZI

Katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2021/2022 (Januari - Machi, 2022), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoa wa Simiyu imekekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

2. UZUIAJI RUSHWA

Katika kipindi hiki TAKUKURU Mkoa wa Simiyu ilijikita katika **Kuzuia Rushwa** kwenye miradi mitano ya barabara inayotekelezwa na TARURA katika Mkoa mzima wa Simiyu yenye thamani ya Shilingi **3,146,927,070** kama ifuatavyo:-

- Maswa Mjini – mama Ngojea, makaburini-market square, Mwagala-Chuo cha Uganga (1 km) kwa kiwango cha lami yenye thamani ya Sh.**499,999,270/=**
- Barabara ya MADECO – kumalija, Stendi mpya (1km) kwa kiwango cha lami yenye thamani ya Sh.**499,935,000/=**
- Barabara ya Somanda – Isakalyamahela 17.17km, Sanungu – Ng'wang'wali 2km, Mahaha - Matale 2km na Kalavati la Senani yenye thamani ya Sh. **446,992,800/=**

- Barabara ya Mwambegwa - Sapa 4km, Mwamanoni-Mwangikulu 9.8km, Mwanduitinje - Isangijo 9.42km, Tindabuligi - Longalonigha 5km, Bukundi-Mwanjolo Senta 1.27km yenye thamani ya Sh. **460,842,990/=**
- Barabara ya Sigala – Badugu 9.7km yenye thamani ya Sh. **500,000,000/=**

Aidha miradi hiyo inaendelea vizuri na utekelezaji na hakuna kasoro yotote iliyobainika hadi sasa.

Katika kipindi hiki TAKUKURU ilifanya warsha na wadau wa elimu na kwa pamoja tuliweka mikakati ya namna ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika katika uchambuzi wa mfumo wa Vihatarishi vya Rushwa ya Ngono katika Sekta ya elimu ikiwemo kulifanya suala la Rushwa ya Ngono kuwa agenda ya kudumu katika vikao kuanzia ngazi ya halmashauri hadi shuleni pamoja na kuanzisha dawati la malalamiko ya Rushwa ya Ngono.

3. UCHUNGUZI

TAKUKURU mkoa wa Simiyu kwa kipindi cha robo ya tatu; Januari – Machi, 2022 tumepokea **taarifa 57** ambapo kati ya hizo **40** zilihusu rushwa na **17** hazihusiani na masuala ya rushwa.

Kati ya taarifa **17** ambazo hazikuhusu masuala ya rushwa taarifa **15** watoa taarifa walishauriwa na kuelimishwa na taarifa **02** zilihamishiwa idara zingine. Aidha kati ya taarifa **36** zilizohusu rushwa, **8** uchunguzi umekamilika ambapo **02** watuhumiwa wameshafikishwa mahakamani na **06** wanatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote kuanzia sasa. Taarifa **28** zinaendelea na Uchunguzi.

Zifuatazo ni Idara zinazolalamikiwa kutokana na taarifa 57 zilizopokelewa;

NA	IDARA	IDADI	MAENEO YALIYOLALAMIKIWA	IDADI
1.	Halmashauri	38	Idara ya Utawala	05
			Idara ya Elimu	05
			Maendeleo ya jamii	01
			Ustawi wa Jamii	01
			Maji	02
			Idara ya Afya	02
			Watendaji wa kata na Vijiji	05
			Maliasili	01
			Wanyamapori	03
			Kilimo	01
			Ardhi	03
			Ujenzi	01
			Ushirika	08
2.	Maeneo mbalimbali	15	Watu binafsi	06
			Polisi	01
			Mahakama	04
			TANESCO	01
			TARURA	02
			Ulinzi	01

Kesi zinazoendelea mahakamani **ni 13** kati ya hizo kesi mpya **ni nne (4)** na katika kipindi hiki **kesi tatu (3)** ziliamuliwa mahakamani na Jamhuri kushinda kesi zote.

4. ELIMU KWA UMMA

Taasisi imeendelea na jukumu lake la kuelimisha umma huku ikitoa kipaumbele kuelimisha wananchi wote kushirikiana na TAKUKURU katika **Kuzuia vitendo vya Rushwa** kwa kutumia Vyombo vya habari kwa kurusha vipindi vya redio 07, Mikutano ya Hadhara (TAKUKURU INAYOTEMBEA) 36, Maonesho 03, Semina 08 pamoja na kuimarisha klabu 64 za Wapinga Rushwa katika shule za sekondari na msingi katika mkoa wa Simiyu.

5.0 MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA

Katika maadhimisho ya wiki ya Sheria nchini yaliyofanyika kuanzia tarehe 23/01/2022 hadi 01/02/2022, TAKUKURU Mkoa wa Simiyu tulitumia maonyesho haya kufanya maonyesho ya uelimishaji umma ambayo yalijumuisha ugawaji wa vipeperushi, majarida na utoaji wa elimu ya rushwa kwa wananchi.

6.0 MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI MACHI 8, 2022

Katika kuelekea maadhimisho ya siku ya wanawake duniani, mnamo tarehe 04/03/2022 TAKUKURU Mkoa wa Simiyu tulitoa elimu ya **Kupinga Rushwa ya Ngono** kupitia kipindi cha **Asubuhi tena** kinachorushwa kila siku ya Ijumaa kuanzia saa 2:00 – 3:00 asubuhi kupitia Radio BARIADI FM iliyopo Bariadi Mjini. Mnamo tarehe 8/3/2022 tulishiriki Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo kimkoa yaalifanyika katika Wilaya ya Itilima ambapo TAKUKURU Mkoa wa Simiyu tulishiriki kwa kutoa elimu ya Kupinga Rushwa ya Ngono ambayo ni kikwazo kikubwa katika kukifikia Kizazi cha Haki na Usawa kwa Maendeleo Endelevu kwa umma uliokusanyika katika maadhimisho hayo.

Sambamba na kushiriki maadhimisho hayo pia watumishi wa kike wa TAKUKURU mkoa mzima wa Simiyu tulitoa misaada ya taulo za kike kwa wanafunzi wa kike wenye mazingira magumu katika shule ya Sekondari ya Itilima pamoja na vifaa vya usafi. Aidha tuliitumia pia siku hiyo kuimarisha klabu ya wapinga rushwa ya shule hiyo kwa kutoa elimu kuhusu rushwa ya ngono na madhara yake kwa wanafunzi wote wa kike wa shule hiyo, kwamba moja kati ya madhara yake ni udhalilishaji wa utu wa mwanamke na kuwa Rushwa ya Ngono pia imekuwa kichocheo cha kukuza na kueneza magonjwa ya zinaa hususan ugonjwa wa UKIMWI.

VIPAUMBELE KWA KIPINDI CHA APRILI – JUNI 2022

Pamoja na utekezaji wa majukumu yetu ya kawaida pia tumejiwekea malengo ya kutekeleza vipaumbele vifuatavyo vinavyolenga KUZUIA VITENDO VYA RUSHWA VISITOKEE:-

I. Kuongeza kasi ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ili kuziba mianya ya rushwa na ufujaji hasa katika Ujenzi wa miradi ya maendeleo ambapo Serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi. Sanjari na kudhibiti mianya ya rushwa na ubadhilifu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Halmashauri zetu lengo likiwa ni kuzisaidia Halmashauri kuweza kujiwezesha kimapato ili kuweza kutekeleza majukumu yao hasa ya kuendeleza ustawi wa jamii
II. Kuongeza kasi ya uelimishaji umma kwa kutumia njia mbalimbali hasa sanaa na michezo.
III. Kuongeza kasi katika kufanya chambuzi za mifumo hasa katika maeneo yanayolalamikiwa zaidi kama maeneo ya utoaji wa huduma kwa wananchi na katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
IV. Tutaendelea kuelimisha jamii na hususani kundi la vijana kupitia ushirikiano uliopo kati ya TAKUKURU na SKAUTI – **TAKUSKA.**

7.0 HITIMISHO

Ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wana Simiyu wote ambao wamekuwa na wanaendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU kwa kutoa taarifa ambazo zimekuwa zikifanikisha kuwabaini wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na hatimaye hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao.

Ninachukua fursa hii pia kuwakumbusha wote kuwa mapambano dhidi ya rushwa ni ya kila mwana Simiyu. Ili kuufanya Mkoa wetu kuwa sehemu isiyokuwa na Rushwa ni wajibu wa kila mmoja wetu kuona umuhimu wa kushiriki kikamilifu katika mapambano haya.

IMETOLEWA NA:

JANETH MACHULYA

MKUU WATAKUKURU (M)

SIMU: 0738150203